JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

## KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

www.kazi.go.tz

Toleo la 9 | Disemba, 2022



*Scan kusoma Jarida kidigitali*




# Waajiri Waaswa Kuzingatia Sheria na Kutoa Mikataba ya Kazi

Waajiri nchini wametakiwa kuzingatia Sheria na kutoa mikataba ya kazi kwa kazi zinazostahili mikataba badala ya kuwafanyisha watu kazi kama vibarua kwa kazi ambazo wangeweza kupata mikataba ya kazi.

Rai hiyo imetolewa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango, Disemba 2, 2022 wakati wa hafla ya utoaji Tuzo za Mwajiri Bora wa Mwaka 2022 zinazoratibiwa na Chama cha Waajiri Nchini (ATE) iliyofanyika katika ukumbi wa Mlimani City Jijini Dar es Salaam.

Aidha, amewasisitiza waajiri kuzingatia Sheria zilizopo kuhusu ajira kwa wageni ikiwemo kuhakikisha nafasi zisizo za kitaalamu au ambazo utaalamu wake unaweza kupatikana hapa nchini hazitolewi kwa wageni.
Vilevile, amewataka waajiri kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na wakati ikiwa ni pamoja na kutoa posho, tuzo na motisha mbalimbali ili kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi bora katika taasisi, kuwapandisha vyeo na kuwapatia stahili zinazoendana na nafasi zao.

Pia, Makamu wa Rais ameagiza Wizara ya Kazi kutoa elimu kwa wafanyakazi na waajiri nchini ili waweze kujua haki zao pamoja na kuhakiki aina ya mikataba inayotolewa kwa lengo la kukidhi vigezo vyote muhimu ikiwa ni pamoja na kuainisha wajibu na haki za mwajiri na waajiri kwenye masuala ya afya, likizo, ulemavu, mafao na migogoro.

Sambamba na hayo, amewataka waajiri kutumia tuzo hizo kama chachu ya kuboresha mazingira ya mahala pa kazi na kuhamasisha utendaji wenye tija kwa manufaa ya Taasisi zao na maendeleo ya nchi kwa ujumla.



## Serikali Yakamilisha Upangaji wa Kima Cha Chini Mshahara Sekta Binafsi

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako amewaeleza Waajiri kuwa Serikali imekamilisha upangaji wa kima cha chini cha Mshahara katika sekta binafsi na kima hicho tayari kimetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 687 la tarehe 25 Novemba, 2022.

Waziri Ndalichako amesema hayo wakati wa hafla ya Utoaji Tuzo za Mwajiri wa Mwaka 2022 zinazoratibiwa na chama cha Waajiri Nchini (ATE) ambapo tukio hilo lilifanyika katika ukumbi wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam.

“Naomba nitumie tukio hili kutangaza rasmi kuwa Serikali imekamilisha upangaji wa Kima cha Chini cha Mshahara sekta binafsi na kima hicho tayari kimeshatangazwa,”

“Kima hicho kitaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 01 Januari, 2023 na ikumbukwe kwamba kwa miaka 9 iliyopita toka mwaka 2013 kulikuwa hakuna tamko rasmi la kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi,”



# Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu Wazinduliwa

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imezindua mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania.

Uzinduzi huo umefanyika kwenye Kilele cha Maadhimisho ya Watu wenye ulemavu Duniani ambapo Kitaifa yaliyofanyika Jijini Arusha, Disemba 3, 2022.

Waziri Ndalichako ameeleza kuwa, hali ya huduma na ustawi kwa Watu wenye Ulemavu ulimwenguni kote inahitaji kuwekewa mipango na mikakati mahususi ya kuzipatia ufumbuzi changamoto ili kuhakikisha kundi hilo haliachwi nyuma.

“Madhumuni ya Mwongozo huu ni kutoa mwelekeo, miongozo na maelekezo kwa Viongozi na watendaji wa Serikali pamoja na wadau wengine katika kuchochea maendeleo na ustawi wa Watu wenye Ulemavu kwa kuongeza hatua za ujumuishwaji na kutoa huduma bora kwao ili kuwawezesha kukabiliana na changamoto za kimaisha zitokanazo na zinazochochewa na ulemavu walionao.

Aidha, Waziri ndalichako amewataka wadau kutekeleza kikamilifu Mwongozo huo wa kukuza Ujumuishwaji na kuimarisha huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini kwa ajili ya maendeleo ya kundi hilo na taifa kwa ujumla.

Aliongeza kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuyapa kipaumbele masuala ya Watu wenye Ulemavu nchini katika nyanja zote ikiwemo Afya, Elimu, uwezeshwaji wa kiuchumi, huduma za marekebisho, michezo na utamaduni pamoja na shughuli za kisiasa na uongozi.

Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani mwaka 2022 ni “**Suluhisho la Mabadiliko kwa ajili ya Maendeleo Jumuishi: Nafasi ya Ubunifu katika kuchagiza dunia inayofikika na yenye usawa**”




## Endeleeni kuchangia Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI - Katambi

Naibu Waziri Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Patrobas Katambi ameiasa jamii na wadau kuendelea kuchangia fedha katika mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWI (ATF) ili kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za afua za UKIMWI nchini.

Ameyasema hayo tarehe 27 novemba, 2022 wakati akihutubia kwa niaba ya Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa kwenye Shughuli za mbio za nyika (Marathon) za kuchangia mfuko huo.

Alisema kustawi kwa mfuko huu kutasaidia kupunguza utegemezi wa rasilimali fedha kutoka kwa wahisani wa nchi za kigeni na kueleza kuwa uwepo wa mfuko imara unatupa uhakika wa uendelevu wa afua za UKIMWI nchini.

Mhe. Katambi aliwapongeza washiriki wote wa mbio hizo huku akotoa rai kwa jamii kuendelea kujitokeza kuchangia mfuko huo kuwa na uhakika wa fedha katika utekelezaji wa afua za masuala ya UKIMWI.

"Kipekee, niwashukuru Wadhamini na Washiriki wote wa Mbio hizi za ATF Marathon 2022 Lindi. Asanteni sana kwa kuchangia Mfuko huu na kushiriki mbio hizi za Marathon, natoa wito kwa Makampuni, Asasi mbalimbali na wananchi wote kuendelea kuhamasika kuchangia mfuko wetu kupitia akaunti ya Benki namba 20110033895 iliyopo Benki ya NMB na namba za simu ya mkononi 0684 90 90 90 kwa ajili ya kuboresha na uendelevu wa huduma za kudhibiti VVU na UKIMWI na hivyo, kuimarisha afya na kuokoa maisha ya Watanzania,"

Serikali kwa kushirikiana na Wadau inafanya juhudi kubwa kuuimarisha Mfuko huu, hususan kuufanya uwe na chanzo cha uhakika na endelevu na kuimarisha usimamizi wake ili kukabilina na changamoto zinazoukabili Mfuko huo kwa sasa.

Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI mwaka huu 2022 ni “IMARISHA USAWA”.





## Wadau Watoa Maoni kuhusu Rasimu ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2022

Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imepokea maoni kuhusu Rasimu ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii kutoka kwa wadau wa sekta ya hifadhi ya jamii wakati wa kikao kazi kilichofanyika jengo la OSHA, leo tarehe 06 Disemba, 2022, jijini Dodoma.

Aidha, hatua ya maandalizi ya Sera hiyo mpya ni kufuatia Sera ya awali ya hifadhi ya jamii ya mwaka 2003 kutofanyiwa mapitio/maboresho kwa muda mrefu, hali iliyopelekea uhitaji wa sera hiyo mpya ambayo itaendana na mabadiliko mbalimbali katika sekta ya hifadhi ya jamii.

Wadau wa Sekta hiyo wameweza kutoa maoni juu ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2022 katika Kikao kazi hicho kilichoongozwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu.

Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kupitia Idara ya Hifadhi ya Jamii na Idara ya Sera na Mipango zinaratibu maandalizi ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2022.

Wadau walioshiriki kikao kazi hicho ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

KATIBU MKUU
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**
Mji wa Serikali, **Mtumba**
Mtaa wa Kazi S.L.P 2890
40411 **DODOMA, Tanzania**
Barua pepe: *ps@kazi.go.tz*
**www.kazi.go.tz**